



TAARIFA KWA VYOMBO VYA HABARI.

Serikali kupitia Wakala ya Serikali Mtandao (eGA) imeunganisha taasisi za ‘Serikali 72 kwenye mfumo wa simu zenye itifaki ya intaneti (*Internet Protocol* (IP) ambazo zinatumia intaneti kuziwezesha taasisi hizo kuwa na mawasiliano yaliyo bora, salama na kupunguza gharama za mawsiliano Serikali.

Taasisi hizo 72 zinajumuisha Wizara, Idara zinazojitegemea na Wakala za Serikali zimeunganishwa na Mtandao wa Mawasiliano wa Serikali yaani '**Government Communication Network (Govnet)**' unaouwezesha mfumo wa simu hizo kufanya kazi kwa ufanisi ambapo mtumishi wa taasisi moja katika taasisi hizo anaweza kupiga simu kwenda taasisi nyingine ya nje ikawa kama umepiga simu ya '**extension**' ndani ya ofisi moja.

Aidha, Taasisi za umma zitanufaika moja kwa moja na simu hizo kwa kuwa, taasisi hizo zitaweza kubadilishana taarifa kupitia mtandao mmoja tu wa Mawasiliano wa Serikali kwa usalama na uhakika. Pia simu hizo zitawawezesha watumishi wa taasisi mbalimbali kufanya mkutano kwa njia ya simu wakiwa kwenye ofisi zao na hivyo kuokoa muda na gharama za usafari.

Hata hivyo, taasisi za umma zilizopo katika mtandao wa mawasiliano wa Seikali zitaendelea kuwasiliana na taasisi zilizo nje ya mtandao huo kwa kupitia mtoa huduma wa simu za mezani (PSTN Provider) kama vile TTCL.

Hivyo, Wakala ya Serikali Mtandao (eGA) inazishauri Taasisi hizo zilizounganishwa na mfumo wa simu hizo kuzitumia katika kazi zao za mawasiliano ya kila siku ili kuboresha utendaji kazi na kupunguza gharama za mawasiliano Serikalini.

xxxxxxxxxxxxxxxxxxxxxxxxxxxxx MWISHO xxxxxxxxxxxxxxxxxxxxxxxx

Imetolewa Na:
SUZAN MSHAKANGOTO
MENEJA HABARI, ELIMU NA MAWASILIANO
WAKALA YA SERIKALI MTANDAO